**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

National Development Plan | Strategy and Plans Development Books

2018

# Mkakati wa Serikali wa Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kutekeleza Miradi yenye Kuchochea Upatikanaji wa Mapato ili ziweze Kujitegemea,2018

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/758

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# MKAKATI WA SERIKALI WA KUZIWEZESHA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KUTEKELEZA MIRADI YENYE KUCHOCHEA UPATIKANAJI WA MAPATO ILI ZIWEZE KUJITEGEMEA



IMETOLEWA NA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO,
IDARA YA BAJETI YA SERIKALI

JANUARI, 2018

# MKAKATI WA SERIKALI WA KUZIWEZESHA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KUTEKELEZA MIRADI YENYE KUCHOCHEA UPATIKANAJI WA MAPATO ILI ZIWEZE KUJITEGEMEA

**Wizara ya Fedha na Mipango**
**S.L.P. 2802**
**DODOMA, TANZANIA**
**Simu: +255-26-2963101**
**Fax: +255-26-2963101**
**Tovuti- http://www.mof.go.tz**

Wizara ya Fedha na Mipango
Idara ya Bajeti ya Serikali
S.L.P. 2802,
DODOMA
TANZANIA

**© Wizara ya Fedha na Mipango, 2018**

**ISBN 978-9987-829-16-3**

Toleo la kwanza, 2018

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Kitabu hiki kwa ajili yoyote kama vile kieletroniki, kurudufu nakala, kurekodi au kwa nia yoyote nyingine bila idhini ya mwandishi au Wizara ya Fedha na Mipango, Idara ya Bajeti ya Serikali.

# YALIYOMO

UTANGULIZI....v

1.0 LENGO NA MADHUMUNI YA MKAKATI....1

2.0 HALMASHAURI ZINAZOLENGWA....2

3.0 MIRADI INAYOLENGWA....3

4.0 UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KUTEKELEZA MKAKATI....5

5.0 WAHUSIKA KATIKA UTARATIBU HUU....5

5.1 Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango....5

5.2 Majukumu ya OR-TAMISEMI....6

5.3 Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa....6

5.4 Majukumu ya Halmashauri husika....7

6.0 MATOKEO TARAJIWA YA MKAKATI HUU....8

7.0 HITIMISHO....10

VIAMBATISHO....12

# UTANGULIZI

Ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendelea kutumia fursa za kimapato zilizopo katika maeneo yao na hivyo kutoa huduma bora zaidi na zenye uhakika kwa wananchi. Ili kufikia lengo hili Serikali imeandaa Mkakati maalum kwa madhumuni ya kuziwezesha Halmashauri kujitegemea kimapato. Mkakati huu umeelezwa pia katika Mwongozo wa Uandaaji Mipango na Bajeti 2018/19-2020/21.

Katika kutekeleza Mkakati huu, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuhakikisha zinatumia kwa ukamilifu fursa za kimapato zilizopo katika maeneo yao na hivyo kuongeza uwezo wa kujitegemea kimapato. Katika kufanikisha lengo hili, ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa kubuni na kuandaa kwa umakini na utaalam Miradi ambayo inatarajiwa kuongeza uwezo wa Halmashauri kimapato. Miradi hii itagharamiwa na Serikali Kuu kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

Aidha, kwa kutambua kuwapo kwa Halmashauri zenye fursa na changamoto tofauti, matumizi mazuri na yenye tija ya fursa katika vyanzo vya mapato yataziwezesha Halmashauri zenye fursa kubwa na vyanzo vya uhakika kujijengea uwezo mkubwa na kujitegemea na hivyo kuiwezesha Serikali kuongeza nguvu na msukumo katika Halmashauri zenye uhitaji zaidi.

Aidha, ni muhimu kupitia kwa umakini viambatisho Na. 1 na 2 ambavyo vimebainisha vigezo pamoja na mwongozo wa sababu za kuwepo kwa vigezo hivyo. Ili kuweza kufaidika na utaratibu huu, Halmashauri zinatakiwa kuzingatia na kukidhi vigezo hivyo.

Ni matumaini yangu kuwa wadau mbalimbali watasoma na kuzingatia maelezo yaliyomo katika Kijitabu hiki ili kuweza kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

**Doto M. James**
**KATIBU MKUU NA MLIPAJI MKUU WA SERIKALI**

## 1.0 LENGO NA MADHUMUNI YA MKAKATI

Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali hutegemea pia upatikanaji wa mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali. Kwa upande wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ruzuku kutoka Serikali Kuu huchangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa bajeti hizo. Takwimu zinaonesha kwamba bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa hutegemea ruzuku hii kwa zaidi ya asilimia 88.

Aidha, zipo Sheria zinazoweka utaratibu na vigezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweza kujiendesha kwa viwango tofauti. Vile vile, Sheria hizo zinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa na uhakika wa mapato yanayotarajiwa kukusanywa kama kodi, ushuru au tozo nyingine zenye kutosheleza utoaji wa huduma muhimu pamoja na uendeshaji wa shughuli za Serikali katika maeneo husika.

Hata hivyo, pamoja na vigezo hivyo vya kibajeti; Serikali Kuu imeendelea kuwa chanzo kikubwa cha mapato katika kugharamia utekelezaji wa majukumu mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuwapo kwa fursa nyingi zinazoweza kutumika kuanzisha, kuimarisha na kuboresha vyanzo vya mapato na hivyo kuongeza uwezo wa kujitegemea na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa kuzingatia sababu hizi, Wizara ya Fedha na Mipango imeanzisha utaratibu kwa Halmashauri mbalimbali kufanya mawasilisho ya miradi yao ya kimkakati katika eneo la kujijenga kimapato. Miradi inayolengwa kuwasilishwa ni ile yenye kujenga uwezo wa kifedha na kuongeza mapato katika Halmashauri kwa madhumuni ya kujitegemea na kuboresha utoaji wa huduma.

Msingi wa utaratibu huu unatokana na ukweli kwamba upatikanaji wa mapato ya kutosha na yenye uhakika katika Halmashauri ni nguzo imara katika kuboresha utoaji huduma nzuri na zenye uhakika kwa wananchi. Aidha, mkakati huu unalenga katika kutatua changamoto za mapato katika ngazi ya Halmashauri. Changamoto hizi ni pamoja na uwezo mdogo wa kubaini na kutumia fursa zilizopo pamoja na usimamizi hafifu katika ukusanyaji, utunzaji na matumizi ya mapato ambazo zina athari katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kutokana na sababu hizi pamoja na kutambua kuwapo kwa Halmashauri zenye fursa na changamoto tofauti, matumizi mazuri na yenye tija ya fursa hizi katika vyanzo vya mapato yataziwezesha Halmashauri kuwa na vyanzo vya uhakika ili kujijengea uwezo wa kujitegemea na hivyo kuiwezesha Serikali Kuu kuongeza nguvu na msukumo katika Halmashauri zenye uhitaji zaidi.

## 2.0 HALMASHAURI ZINAZOLENGWA

Halmashauri zitahusishwa katika Mpango huu kwa kukidhi vigezo. Kipaumbele katika ushirikishaji wa Halmashauri utazingatia vigezo vifuatavyo:-

a) Halmashauri ambazo zimetenga fedha katika bajeti zao;

b) Halmashauri zenye fursa za uhakika wa mapato zinazohitaji kuongezewa nguvu ya kifedha kwa ajili ya uwekezaji;

c) Halmashauri zenye fursa za kimapato lakini vyanzo vyake vinahitaji msukumo wa Serikali Kuu ili viweze kukamilika na kuingiza mapato;

d) Halmashauri ambazo tayari ziko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa miundo mbinu

ya uingizaji mapato lakini zimeshindwa kukamilisha kutokana na changamoto za kifedha;

e) Halmasahuri mpya ambazo hazina vyanzo vya uhakika vya mapato;

f) Halmashauri ambazo kimuundo vyanzo vyake vinahitaji uwekezaji mkubwa;

g) Halmashauri ambazo zimekamilisha taratibu zote za maandalizi ya awali ikiwa ni pamoja na kuwa na umiliki halali wa maeneo hayo, kukamilisha taratibu za fidia iwapo zinahusika, na kwamba maeneo husika tayari yameainishwa na yako tayari kwa uwekezaji;

h) Halmashauri ambazo ziko katika hatua mbalimbali ya majadiliano katika utaratibu wa ubia kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP).

i) Halmashauri zenye miradi inayokidhi vigezo vya kukopeshwa kutoka katika Taasisi za Fedha (Bankable Projects).

## 3.0 MIRADI INAYOLENGWA

Pamoja na Halmashauri kupewa kipaumbele katika kuwezeshwa ili zijitegemee kama ilivyoanishwa kwenye Kitabu hiki, vigezo vifuatavyo vitazingatiwa kabla Serikali haijatoa fedha katika miradi husika:-

a) Miradi ambayo inakidhi malengo yaliyomo katika Mpango Mkakati wa Halmashauri na ipo kwenye bajeti;

b) Miradi iliyofanyiwa upembuzi yakinifu na ina Andiko la Mradi ambalo limekamilika;

c) Miradi yenye fursa za uhakika za mapato;

d) Miradi ambayo Halmashauri ina uwezo wa kuiendesha kwa ufanisi;

e) Miradi ambayo imezingatia dhana ya viwanda jumuishi na endelevu, kuongeza thamani na kuboresha mfumo wa ufungaji;

f) Miradi ambayo inaongeza ajira, kukuza kipato na kuboresha maisha ya wananchi.

Aidha, pamoja na kubainisha miradi hii, Halmashauri zitatakiwa pia kubainisha kwa kina yafuatayo:-

i) Mapato yanayotegemewa kutokana na mradi husika katika muda mfupi, wa kati na mrefu pamoja na kuwasilisha taarifa za ukaguzi wa fedha zilizohakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG);

ii) Mkakati wenye muda maalum kwa Halmashauri wa kutumia vyanzo hivi vya mapato katika kuongeza mapato, kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu na kuweza kujiendesha;

iii) Mikakati ya kutumia mapato yatokanayo na miradi hiyo katika kuboresha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii katika Halmashauri husika.

## 4.0 UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KUTEKELEZA MKAKATI

Wizara ya Fedha na Mipango itaratibu utekelezaji wa mkakati huu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali muhimu. Wadau hawa watahusika katika hatua za awali za uchambuzi, ukamilishaji na ufuatiliaji. Wadau hao ni pamoja na OR-TAMISEMI na Sekretarieti za Mikoa.

Aidha, maelekezo ya jumla yafuatayo yatazingatiwa katika utekelezaji wa mkakati huu:-

i) Halmashauri zitakazopata fedha hizo zitasaini Mikataba ya Utekelezaji na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na OR-TAMISEMI;

ii) Fedha hizo zitatumika kwa madhumuni na malengo kama yalivyoainishwa katika Mikataba ya Utekelezaji;

iii) Uhamisho wa fedha kutoka katika miradi hii ya kimkakati hautaruhusiwa;

iv) Halmashauri zitakazoshindwa kutekeleza Mikataba hiyo zitachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu.

## 5.0 WAHUSIKA KATIKA UTARATIBU HUU

Wahusika katika utaratibu huu ni pamoja na:- Wizara ya Fedha na Mipango, OR-TAMISEMI; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 5.1 Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango

i) Kuandaa utaratibu na mwongozo wa uchambuzi na vigezo;

ii) Kufanya uchambuzi, tathmini na uainishaji wa miradi inayokidhi vigezo vilivyowekwa;

iii) Kuandaa utaratibu na kutoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo;

iv) Kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na usimamizi kwa madhumuni ya kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha hizo na malengo yaliyokusudiwa yanazingatiwa;

v) Kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria na taratibu pale ambapo malengo yaliyokusudiwa yamekiukwa;

## 5.2 Majukumu ya OR-TAMISEMI

i) OR-TAMISEMI kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika uratibu wa jukumu hili.

ii) Kushiriki katika uchambuzi na tathmini;

iii) Kufanya ufuatiliaji na usimamizi kwa madhumuni ya kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha hizo na malengo yaliyokusudiwa yanazingatiwa;

iv) Kuchukua hatua stahiki pale ambapo malengo yaliyokusudiwa yamekiukwa.

## 5.3 Majukumu ya Sekretarieti za Mikoa

Katika utaratibu huu, Ofisi za Sekretarieti za Mikoa zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

i) Kufanya uchambuzi wa awali na kuzipanga Halmashauri zilizopo ndani ya Mikoa husika kwa kuzingatia vigezo vilivyotajwa katika Kitabu hiki;

ii) Kusimamia na kuhakikisha Halmashauri hizo zinaandaa nyaraka pamoja na vielelezo stahiki kwa ajili ya uwasilishaji;

iii) Kuzipanga Halmashauri katika makundi kwa kuzingatia fursa na uhitaji kama ilivyofafanuliwa katika Kitabu hiki;

iv) Kushiriki na kutoa tathmini katika uchambuzi wa Kimkoa;

v) Kusimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa miradi itakayopatiwa fedha;

vi) Kuhakikisha malengo na matumizi yanazingatia vigezo na madhumuni.

## 5.4 Majukumu ya Halmashauri

i) Kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa, kuchambua na kuandaa miradi ya kimkakati;

ii) Kuzingatia kuwasilisha miradi katika Sekretarieti za Mikoa kwa uchambuzi wa awali pamoja na taratibu zinazohusika;

iii) Kuandaa nyaraka na vielelezo vinavyohitajika kwa ajili ya uwasilishaji na uchambuzi;

iv) Kuhakikisha miradi inayopatiwa fedha inatekelezwa na kukamilika katika muda uliopangwa;

v) Kuhakikisha miradi husika inatekelezwa na kusimamiwa kikamilifu na kuiwezesha Halmashauri

kujijenga kimapato na kujitegemea;

vi) Kuhakikisha mapato yatokanayo na miradi yanasimamiwa kikamilifu na kutumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa.

vii) Kurejesha fedha Hazina ambazo zitatumika kinyume na malengo ya mradi pamoja na kuingiza mapato yatokanayo na miradi hii kwenye bajeti na kufuata taratibu zote za kibajeti kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

## 6.0 MATOKEO TARAJIWA KATIKA MKAKATI HUU

Kwa kuzingatia uchambuzi huu, matokeo tarajiwa ni kama ifuatavyo:-

i) Serikali Kuu kujielekeza katika miradi muhimu ya kujenga na kuimarisha mapato ya Halmashauri na kuziwezesha Halmashauri kujitegemea;

ii) Serikali Kuu kuongeza nguvu na msukumo zaidi kwenye Halmashauri zenye uhitaji mkubwa. Aidha, zile zenye fursa nzuri kimapato kuwezeshwa kutumia vizuri fursa hizo na kujiendesha zenyewe;

iii) Kuziwezesha Halmashauri kujielekeza kwenye miradi yenye tija, kuongeza ajira na kusaidia kimapato katika utoaji wa huduma mbalimbali;

iv) Kuziwezesha Halmashauri ambazo zinahitaji msukumo mdogo wa kifedha ili ziweze kuendesha vyanzo vyake vya mapato na kujitegemea;

v) Kuziwezesha Halmashauri ambazo zinahitaji uwekezaji mkubwa ili kuweza kujikusanyia mapato na kujiendesha;

vi) Kuziwezesha Halmashauri ambazo mapato yake hayakidhi kujiendesha;

vii) Kuwapo kwa orodha ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika mwaka wa fedha husika.

viii) Kuwapo kwa mapendekezo ya utekelezaji wa miradi hii katika Bajeti za Halmashauri kwa kuzingatia utaratibu wa MTEF.

ix) Serikali Kuu kuelekeza fedha katika maeneo mengine kutokana na kupungua kwa utegemezi wa Halmashauri ikiwamo miradi ya Kitaifa ya Kimkakati (Strategic Projects).

## 7.0 HITIMISHO

Utoaji wa fedha utaelekezwa katika miradi iliyokidhi vigezo vilivyoainishwa. Aidha, inatarajiwa kwamba miradi itakayopatiwa fedha itatekelezwa na kukamilika katika muda uliopangwa. Halmashauri zitatakiwa kutekeleza na kuisimamia kikamilifu miradi hiyo ili hatimaye ziweze kujitegemea kimapato na kutoa nafasi kwa Halmashauri nyingine kufaidika na utaratibu huu.

Aidha, kwa kupitia utaratibu huu utawezesha kuziweka Halmashauri katika makundi tofauti kama ifuatavyo:-

i) Halmashauri zilizokidhi vigezo,

ii) Halmashauri zitakazopewa maelekezo ya kufanya marekebisho ili zikidhi vigezo,

iii) Halmashauri ambazo hazijakidhi vigezo na zipo mbali na wigo wa kufikiriwa kupewa nafasi ya kukidhi au kujirekebisha. Maelekezo na utaratibu maalum utatolewa kwa Halmashauri zitakazoangukia katika kundi hili.

Ni muhimu pia kuzingatia kuwa mapato yatokanayo na miradi hii yatasaidia katika kutoa na kuboresha huduma katika maeneo mengine ikiwamo afya, maji, kilimo na mengineyo. Ofisi za Sekretarieti za Mikoa ambazo kimsingi ndio wachambuzi wa awali wa miradi hii zina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba malengo na madhumuni ya kuwapo kwa mkakati huu yanafikiwa katika maeneo wanayosimamia.

## MAPITIO NA MACHAPISHO YA REJEA


1. *Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015.*

2. *Bajeti ya Serikali: 2015/16, 2016/17 na 2017/18: Wizara ya Fedha na Mipango.*

3. *Mwongozo wa Uandaaji Mipango na Bajeti: 2018/19-2020/21: Wizara ya Fedha na Mipango.*

4. *Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17- 2020/21.*

5. *Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007.*

6. *Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982, Sura 290.*

7. *Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001, Sura 348.*

# VIAMBATISHO (STRATEGIC PROJECT CRITERIA FORMS)

## KIAMBATISHO Na. 1: SPCF 1:
## UCHAMBUZI WA MIRADI YA KIMKAKATI

### A: TAARIFA ZA JUMLA

Mkoa:..............................................................................................................

Jina la Halmashauri:........................................................................................

Jina la Mradi:...................................................................................................

Eneo la utekelezaji wa mradi:..........................................................................

Muda wa utekelezaji wa mradi:.........................................................................

Kiasi cha fedha kinachoombwa (Tshs.):............................................................

### B: VIGEZO, TAARIFA MAHSUSI NA ALAMA

| Na. | Kigezo | Alama % |
|---|---|---|
| 1. | Andiko la Mradi / Biashara. | |
| 2. | Upembuzi yakinifu. | |
| 3. | Mtiririko wa fedha. | |
| 4. | Uwezo wa kuongeza mapato. | |
| 5. | Uwezo wa Halmashauri kusimamia mradi. | |
| 6. | Uthibitisho wa umiliki wa ardhi. | |
| 7. | Uchambuzi wa viashiria vya uhimilivu (SWOT). | |
| 8. | Uwezo na mpango wa Halmashauri kujitegemea. | |
| 9. | Michoro na Usanifu (Detailed Design Study). | |
| 10. | Mpango wa matumizi ya eneo la mradi (Master Plan). | |
| 11. | Hati safi ya ukaguzi wa hesabu. | |
| 12. | Mpango Mkakati wa Halmashauri. | |
| 13. | Nyaraka za mradi na vielelezo kuchambuliwa na kuridhiwa na Sekretarieti ya Mkoa husika. | |
| 14. | Nyaraka za mradi na vielelezo kuchambuliwa na kuridhiwa na OR-TAMISEMI. | |
| | **JUMLA KUU (100%)** | |

## KIAMBATISHO Na. 2: SPCF 3
## MWONGOZO WA VIGEZO NA SABABU

| Na. | Kigezo | *Sababu* |
|---|---|---|
| 1. | Andiko la mradi / biashara | Andiko la Mradi ni wasifu na maelezo yanayoeleza na kutoa picha halisi kuhusu mradi. Taarifa zinazopatikana katika Andiko la mradi ni pamoja na:-<br>- Jina la mradi<br>- Historia ya mradi<br>- Lengo kuu na malengo mahsusi<br>- Umuhimu wa kuwa na mradi (faida kiuchumi na kijamii)<br>- Mpango wa utekelezaji<br>- Muda wa utekelezaji mradi<br>- Uongozi, usimamizi na ufuatiliaji<br>- Masuala mtambuka<br>- Mtaji na rasilimali zingine<br>- Fursa na changamoto zilizopo<br>- Vihatarishi na namna ya kukabiliana navyo<br>- Ajira na namna ya kuwezesha jamii kupunguza umaskini<br>- Mpango endelevu wa mradi<br><br>Taarifa hizi ni muhimu kwani ndio chanzo cha kujenga msingi wa maamuzi ya kuwekeza rasilimali katika kutekeleza mradi husika. |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Upembuzi yakinifu | Mchakato ambao unatoa fursa ya kuchambua na kutathmini kwa kina namna gani utelekezaji wa mradi utaweza kufikia malengo, vigezo, viwango na viashiria kiuchumi na kijamii.<br><br>Upembuzi yakinifu hubainisha/hutoa taarifa kuhusu gharama na faida za uwekezaji, uchambuzi wa thamani ya fedha dhidi ya uwekezaji, uchambuzi wa namna mbalimbali za upatikanaji wa mtaji, riba na marejesho, uchambuzi kuhusu uzalishaji, masoko, na uhimilivu wa mradi.<br><br>Aidha, upembuzi yakinifu hubainisha au hutoa majibu kuhusu sababu za mafanikio, namna mradi unavyoweza kupokelewa na jamii, athari za kimazingira, namna ya kukabiliana na athari za kimazingira na uwezo wa washindani katika soko/mradi husika.<br><br>Taarifa hizi ni muhimu kwa sababu huchangia katika kuamua kutekeleza mradi huu au mwingine. Kwa kuzingatia uhaba wa rasilimali ni lazima na muhimu wakati wote kufanya maamuzi sahihi katika kuamua matumizi ya rasilimali. |
| 3. | Mtiririko wa fedha | Mtiririko wa fedha ni mchanganuo wa mapato na matumizi katika mradi. Mtiririko wa fedha unatakiwa ubainishe kwa namna gani mapato yanakidhi gharama za uzalishaji/matumizi kwa kipindi cha takribani muda wa miaka 3 ya mwanzo.<br><br>Madhumuni ya kigezo hiki ni kujua kama / iwapo mradi utakidhi na utakuwa na mtiririko chanya wa fedha. |
| 4. | Uwezo wa kuongeza mapato | Kuonyesha uwezo wa mradi kuchangia mapato ya Halmashauri. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Uwezo wa Halmashauri kusimamia mradi | Kwa kuzingatia mahitaji ya mradi, kuwepo kwa wataalamu wenye uzoefu wa kusimamia, kuwapo kwa nidhamu ya usimamizi wa fedha na rasilimali pamoja na kuwa na uzoefu wa kusimamia miradi mingine inayofanana. |
| 6. | Uthibitisho wa umiliki wa ardhi | Uthibitisho wa umiliki wa eneo kisheria ili kuepuka migogoro inayoweza kusababisha mradi usitekelezwe kwa wakati. |
| 7. | Uchambuzi wa viashiria vya uhimilivu (SWOT) | Uchambuzi wa viashiria vya uhimilivu utasaidia kubaini fursa, uwezo, changamoto na vikwazo. Vile vile, kubaini mikakati ya kutumia fursa zilizopo na kukabiliana na changamoto zitakazo jitokeza. |
| 8. | Uwezo na Mkakati wa Halmashauri kujitegemea | Lengo ni kutambua uwezo wa Halmashauri katika kukusanya mapato yao ya ndani ikilinganishwa na matumizi yao pamoja na kuonesha mpango kazi wa kupunguza utegemezi kutoka Bajeti Kuu ya Serikali kutokana na kutekelezwa kwa mradi huo. |
| 9. | Michoro na Usanifu (Detailed Design Study) | Kuona uhalisia wa mradi unaoidhinishiwa fedha na uthibitisho wa makisio ya gharama za mradi. |
| 10. | Mpango wa matumizi ya eneo la mradi (Master Plan) | Kuona matumizi sahihi ya eneo la mradi ili kuepuka gharama zisizo za lazima kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya ardhi katika eneo la mradi. |
| 11. | Hati ya ukaguzi wa Hesabu | Uthibitisho wa usimamizi mzuri wa rasilimali na uendeshaji wa Halmashauri kwa kuwa na hati safi ya ukaguzi wa hesabu kutoka Ofisi ya CAG. |
| 12. | Mpango Mkakati wa Halmashauri | Kuzingatia na kuendana na Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015 kwa kutekeleza miradi ambayo iko kwenye Mpango. |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Nyaraka za mradi na vielelezo kuchambuliwa na kuridhiwa na Sekretarieti ya Mkoa husika | Kuzingatia majukumu ya RS katika kusimamia, kuratibu na kufuatilia ufanisi wa utekelezaji wa majukumu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. |
| 14. | Nyaraka za mradi na vielelezo kuchambuliwa na kuridhiwa na OR-TAMISEMI | Kuzingatia majukumu ya OR-TAMISEMI katika kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya kisera na miongozo katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. |

ISBN 978-9987-829-16-3

Kimepigwa chapa na Wizara ya Elimu, Press 'A'
7 Mtaa wa Magogoni, S. L. P. 9121, 11479 Dar es Salaam.
Simu: +255 2110092, Nukushi: +255 2110092, Baruapepe: moepa@moe.go.tz